TANGAZO LA SERIKALI NA. 781 la tarehe 3/11/2023

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetolewachini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE GAWIO KATIKA MRADI WA UENDELEZAJI NA UENDESHAJI WA MIUNDOMBINU YA KISASA YA KONGANI YA VIWANDA KWA KAMPUNI YA SINO TAN KIBAHA INDUSTRIAL PARK YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio Kwenye Gawio Katika Mradi wa Uendelezaji na Uendeshaji wa Miundombinu ya Kisasa ya Kongani ya Viwanda kwa Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park ya mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 25 Agosti, 2023.

Msamaha

2. Kodi yote ya zuio kwenye gawio kwa ajili ya Mradi wa Uendelezaji na Uendeshaji wa Miundombinu ya Kisasa ya Kongani ya Viwanda, inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park, imesamehewa.

Ukomo

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 25 Agosti, 2024.

Dodoma,
19 Octobar, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*